BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Kumi na Nne – Tarehe 21 Mei, 2026
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua Zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa mwaka 2026/2027.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa mwaka 2026/2027.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

109. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Pamoja na kufanyika marekebisho kadhaa ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2024, mabadiliko ya muda wa vikao kutoka saa 3:00 asubuhi mpaka saa 7:00 mchana na kubadilisha kwenda mpaka saa 9:00 mchana sio rafiki kwa wananchi wanaofuatilia Baraza. Wananchi wengi hupata muda wa

kufuatilia Baraza nyakati za jioni kama ilivyokuwa zamani kwa kuwa nyakati za mchana wanakuwa kwenye shughuli zao.

(a) Je, marekebisho hayo ya muda wa vikao yalipata maoni ya wadau kwa upande wa wananchi ambao wanafuatilia vikao vya Baraza.

(b) Je, Afisi ya Baraza haioni haja ya kurejesha muda wa zamani wa jioni ili kuwezesha wananchi kufuatilia vikao vya Baraza baada ya kumaliza shughuli zao za mchana kama ilivyokuwa zamani.

(c) Kwa muda uliowekwa sasa wa kutoka asubuhi mpaka mchana wa saa 9:00, je Afisi ya Baraza haioni kuwa hauna manufaa kwa afya za Wajumbe na watumishi kwa kuwa hakuna kitambo cha kupumzika hata kidogo.

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

52. MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (Jimbo la Ole) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Kwa kuwa Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014 zimempa kila mtumishi wa umma haki ya kupanda daraja na kuongezwa maslahi kila baada ya miaka mitatu ya utumishi wake.

(a) Je, Serikali hutumia vigezo gani katika kuwapandisha daraja watumishi wa umma.

(b) Kwa kuzingatia takwimu ya miaka mitano iliyopita, ni watumishi wangapi waliopandishwa daraja na kwa ngazi zipi.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

280. MHESHIMIWA ALLEY MASOUD ALLEY (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kuna baadhi ya masoko yamejengwa mbali na makaazi ya wananchi likiwemo soko la Kipitacho liliopo Mkoani na kusababisha wananchi wengi kushindwa kufika sokoni na wafanyabiashara kukosa wateja.

Je, Serikali ina mpango gani wa kulishughulikia tatizo hili.

**<u>Wizara ya Fedha na Mipango:</u>**

133. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Mfuko wa Huduma ya Afya Zanzibar (ZHSF) kwa kuweka kifurushi maalum kwa ajili ya Watu Wenye Ulemavu ikijumuisha huduma za marekebisho na vifaa saidizi kwa Watu Wenye Ulemavu.

(a) Je, ni watu wangapi wenye ulemavu wamepatiwa vitambulisho vya huduma ya afya ili waweze kunufaika na kifurushi hicho.

(b) Je, huduma hizo za marekebisho na vifaa saidizi zinapatikana katika ngazi ipi ya hospitali na kwa utaratibu gani.

**<u>Wizara ya Kazi na Uwekezaji:</u>**

147. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Uwekezaji:

Je, Wizara ina utaratibu gani wa kuhakikisha mikataba ya uwekezaji inakuwa wazi na inalinda maslahi ya taifa pamoja na wananchi.

**<u>Wizara ya Maji, Nishati na Madini:</u>**

58. MHESHIMIWA ABDULGHANI ISMAIL ZUBEIR (Jimbo la Malindi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati Na Madini;

Pamoja na jitihada za Serikali kuimarisha huduma za upatikanaji wa maji safi na salama hapa Zanzibar bado kuna baadhi ya sehemu za Mjini zimekuwa na upungufu wa kupatikana huduma hiyo ikiwemo jimbo la Malindi.

Je, ni lini Serikali italipatia ufumbuzi tatizo hili la maji katika maeneo yote ya Mjini.

**<u>Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:</u>**

30. MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (Mwakilishi Jimbo la Ole) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa katika vigezo vya elimu kutoka Diploma kwenda Shahada ya Kwanza (Degree) mwanafunzi anatakiwa awe na angalau ufaulu

wa 3.0 GPA. Tafiti zinaonesha kwa mwaka mmoja kuna idadi kubwa ya wanafunzi ambao ni watumishi wa umma ambao hawajafikia kiwango cha GPA ya 3.0 wanaojiunga na vyuo mbalimbali nchini Uganda.

Kwa nini Serikali haifanyi mazungumzo na Tanzania Commission for Universities (TCU) kulegeza masharti kwa watumishi wa umma ili wabakie kusoma hapa hapa Zanzibar badala ya kubeba mzigo mkubwa wa kuwasomesha watumishi hao nje ya nchi.

368. MHESHIMIWA SAID AZANA MSINGIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Licha ya jitihada kubwa zinazochukuliwa na Serikali katika kuhakikisha mazingira bora na mazuri ya kusomea na kusomesha katika skuli zetu bado kuna changamoto kubwa ya baadhi ya skuli kukosa dahalia ikiwa ni pamoja na skuli ya Uzini.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga dahalia ya kisasa katika skuli ya Uzini.

**<u>Wizara ya Afya:</u>**

394. MHESHIMIWA DKT. NASRA NASSOR OMAR (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa mujibu wa taratibu za mafunzo ya Kada za Afya wahitimu wa Shahada ya Ufamasia wanatakiwa kufanya Mafunzo ya Vitendo (Internship) ya mwaka mmoja katika vituo vilivyopangwa kama Hospitali, Bohari za Dawa na Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar - ZFDA.

Kihistoria wanafunzi wa kada hii pamoja na kada nyengine za afya walikuwa wakilipwa posho ya Mafunzo ya Vitendo katika kipindi chote cha mafunzo. Hata hivyo, utekelezaji wa jambo hilo umekuwa ukichukua sura mpya kila mwaka kwa mfano; mwaka 2023 wanafunzi walilipwa miezi mitatu pekee na kuanzia mwaka 2024 hadi sasa hawajalipwa chochote.

(a) Kwa nini Serikali imesitisha au imeshindwa kulipa posho ya Mafunzo ya Vitendo kwa kada ya Ufamasia, wakati kada nyengine za afya zinaendelea kulipwa kama sheria inavyoelekeza.

(b) Je, kuna ukweli upi kuwa fedha za Mafunzo ya Vitendo kwa miaka hiyo zilitengwa kwenye bajeti ya Serikali, na kwa nini Wafamasia hawakunufaika na fedha hizo.

(c) Kwa nini mafunzo haya yaliposimamiwa na Wakala wa Chakula Dawa na Vipodozi Zanzibar wahitimu wote walilipwa posho zao lakini baada ya kuhamishiwa Wizara ya Afya Wafamasia pekee wanakosa haki hiyo.

421. MHESHIMIWA JUMA HASSAN THABIT (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kituo cha Afya cha Fuoni kimefungwa tokea mwezi wa Februari 2025 kwa ajili ya kufanyiwa ukarabati.

Ni lini ukarabati huo utakamilika ili wakaazi wa jimbo la Fuoni waweze kukitumia kituo hicho.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

252. MHESHIMIWA KHAMIS MOHAMMED AMRAN (Jimbo la Mkoani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Serikali ina mikakati gani ya kuendeleza Utalii wa Bahari katika visiwa vidogo vidogo hasa vilivyopo katika jimbo la Mkoani.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

461. MHESHIMIWA JUMA HASSAN THABIT (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

(a) Kwa kuwa Serikali imefanikiwa kujenga Kituo cha Kimataifa cha Biashara katika eneo la Nyamanzi, je ni matokeo gani chanya yaliyopatikana katika kuongeza pato la taifa hadi kufikia sasa.

(b) Je, kwa kiasi gani wananchi wa Dimani wamefaidika kiuchumi na kituo hicho.

**Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:**

308. MHESHIMIWA MAHFOUDH ABDALLA MOHAMMED (Jimbo la Magomeni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:

Serikali imeunda Wizara maalumu ya Ubunifu na Teknolojia ya Habari ili kuendana na kasi ya dunia ya maendeleo ya teknolojia na

ubunifu wenye kurahisisha upatikanaji wa bidhaa na huduma.

(a) Je, ni ipi mipango ya Serikali ya kuhamasisha na kukuza ubunifu kwa vijana wetu.

(b) Vijana wabunifu wanapitia changomoto za vifaa vya kutendea kazi kama vile CNC Mashine, Leather Cutter na nyenginezo. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwarahisishia vijana kupata nyenzo hizo.

**<u>Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji:</u>**

463. MHESHIMIWA JUMA HASSAN THABIT (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Vijana, Ajira na Uwezeshaji:

Kwa kuzingatia mabadiliko ya kimuundo, kisheria na kiutendaji yanayoendelea tokea kuanzishwa kwa Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (ZEEA) ni dhahiri kuwa taasisi hii imefikia hatua ya kutokuwa na hadhi ya kuendelea kuwa wakala.

(a) Ni lini Serikali itaona kuwa ipo haja na hoja ya kuifanya taasisi hiyo kuwa na hadhi ya Mamlaka kutokana na kuwa na uhusiano wa moja kwa moja wa kiuchumi wa taifa na wananchi wa Zanzibar.

(b) Je, kuna taarifa yoyote ya Utendaji na Tathmini ya Utekelezaji wa Wakala huo (Perfomance and Assessment reports), iliyofanyika inayoonesha mafanikio yake.

**<u>Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:</u>**

145. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Namuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Je, Wizara imeweka utaratibu gani wa kuwapatia mikopo au msaada wa kifedha wavuvi wanawake na vijana ili waweze kuwekeza katika shughuli za uchumi wa buluu.

III. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa mwaka 2026/2027.

Zanzibar,
21 Mei, 2026.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA LA
WAWAKILISHI, ZANZIBAR